

## MAENEO YA UMMA KATI YA KUKUZA FAIDA NA HATARI ZA UKIUKAJI.

Imefasiriwa na

Profesa.Ayman Alasar

Hotuba ya Kwanza.

Shukrani ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote. Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu: **{Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo}** ninashuhudia kuwa hakuna mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mje wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka sala na salamu kwake Mtume pamoja na watu wake na Maswahaba zake na wale wote waliomfuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

**Baada ya utangulizi huo:**

Hakika dini ya Uislamu ni dini ya ujenzi na maendeleo, kwa hakika umekuja ujumbe wa mbinguni ukilingania msingi huo ambapo Anasema Mola Mtukufu: **{Na Musa akamwambia nduguye Haaran: Shika mahala pangu kwa watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu}** na anasema Mola Mtukufu kupitia ulimi wa Nabii Shuaibu - *Amani ya Mungu iwe kwake* – **{Sitaki ila kutengeneza kiasi ninavyo weza. Na sipati kuwezesha haya ila na Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye ninategemea, na kwake Yeye naelekea}**.

Na katika jambo lilsilo na shaka yeyote ndani yake ni kuwa kulinda maeneo ya umma ambayo nchi inayajenga na kuyaboresha ni sura katika sura za ujenzi ambao manufaa yake na faida zake hurejea kwenye jamii yote, hilo ni kwa vile haki ya kunufaika nayo si miliki ya mtu yeyote wala kundi lolote, bali ni miliki ya jamii yote, kama tunavyofaidika sote na hayo maeneo ya umma basi ni jukumu letu sote kuyalinda, na kuzuia mkono wa muharibifu kwa kufanya jaribio lolote lile la kuharibu maeneo hayo au kuyabomoa.

Ni lazima kwa kila anayefanya kazi kwenye maeneo hayo ya umma kutekeleza kazi zake kwa nia safi na umahili mkubwa, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W *“Hakika Mwenyezi Mungu anapenda pindi mmoja wenu anapofanya kazi basi aifanya kwa umakini mkubwa”*, kama vile mwenye kunufaika nayo anapaswa

kuyatumia kwa njia isiyokuwa na madhara ndani yake wala uharibifu wala utumiaji mbaya, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W *“Hakuna kudhuru wala kujidhuru”* kwa sababu hiyo hufikiwa ushirikiano kati ya wananchi kwa njia za kheir na manufaa ya wote, ambapo Anasema Mola Mtukufu: **{Na saidianeni katika wema na ucha-Mungu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui}**.

Kulinda maeneo ya umma ni wajibu wa Kisharia kitaifa na kibinadamu, na wajibu huu hauishii kwenye kuyalinda tu bali unaendelea kwenye kufanya kazi ya kuyakuza na kushiriki kwenye kuyaboresha, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W *“Mambo saba mja anaendelea kulipwa akiwa ndani ya kaburi lake baada ya kifo chake: Mtu kafundisha elimu, au amefukuwa mt, o au kachimba kisima, au amepanda mche wa mtende, au amejenga Msikiti, au amerithisha Msahafu, au ameacha mtoto anayemuomba dua baada ya kufa kwake”*.

Na maana ya kufukuwa mto ni kuupanua, na hupimwa hilo kila mapito ya maji, hivyo ni wajibu wetu kuyasafisha na kuyatanua mapito hayo ya maji, wala sio kuyafanyia uadui wala kuyabana, vile vile hali ni kama hiyo katika swala la barabara kuu ambayo inapaswa kulindwa na wala sio kuifanyia uadua au kuibana kwa wapitaji au kutupia takataka na mfano wake.

Na asiyekuwa na uwezo wa kukuza manufaa ya maeneo haya ya umma basi ni wajibu wake kumuihimiza mwengine kufanya hivyo ikiwa kutekeleza kauli ya Mtume S.A.W *“Hakika mwenye kuelekeza jambo zuri basi ni kama mtenda wa jambo hilo”* ikiwa mtu hawezi basi na azuie mkono wake na vitendo vya uharibifu wa kitu chochote kwenye eneo hilo, ambapo anasema Mola Mtukufu: **{Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi watu wenye kufanya uharibifu}**. Na Anasema pia Mola Mukufu: **{Na Mwenyezi Mungu hapendi uharibifu}**, kama vile ni jukumu letu sisi sote kuwa na shime ya kulinda na kutumia vizuri.

Tunasisitiza kuwa maeneo yote ya umma na yanayomilikiwa na nchi kama vile taasisi shule mahospitali barabara na njia za mawasiliano ni amana iliyo kwenye shingo zetu tutakuja ulizwa sisi sote, hivyo wala haifai kuchafua au kuharibu kwa sura yeyote ile miongoni mwa sura za uharibifu au matumizi mabaya.

\*\*\*\*\*

**Hotuba ya Pili.**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, sala na salamu zimshukie Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na Watu wake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa kulinda maeneo ya umma na kutoyaharibu ni miongoni mwa mambo ya kheir na njia ya mafanikio, hivyo Mtume wetu S.A.W amefanya swala la kuzuia kero ni sehemu ya Imani, na ni moja ya aina za sadaka, na ni katika sababu za kuingia Peponi, ambapo anasema Mtume S.A.W *“Imani inasehemu sabini au sitini, sehemu iliyobora zaidi ni kusema: **Hakuna Mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu**, na sehemu ya chini zaidi ni kuondoa kero barabarani”*. Na anasema S.A.W *“Muislamu wa kweli ni mwenye kuwalinda watu kutokana na ulimi wake na mkono wake”*. Na amesema tena S.A.W *“Hakika nimemuona mtu anazunguka Peponi kwenye mti alioukata sehemu ya barabarani ulikuwa ukiwakera Waislamu”*. Anasema tena Mtume S.A.W *“Kuzuia kero zake kwa watu ni sadaka itokayo kwake kwa ajili ya nafsi yake”*.

Ni mahitaji yetu zaidi kuelewa umuhimu wa maeneo ya umma, na wajibu wa kuyalinda kupitia kupandikiza hisia za majukumu ya kidini na kitaifa ya kulinda nchi na mali zake pamoja na kuendeleza vyanzo vyake, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Basi watakao mcha-Mungu na wakatengenea haitakuwa hofu kwao, wala hawatahuzunika**}.

**Ewe Mwenyezi Mungu tunakumba uilinde nchi ya Misri pamoja na nchi za ulimwengu wa Kiarabu na Kiislamu.**